Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Ofisi ya Makamu wa Rais

# Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini (Ecosystem-based Adaptation for Rural Resilience (EBARR) in Tanzania)

**Mafanikio ya Mradi 2021 - 2022**



© VPO - EBARR Project

# Utangulizi

Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi. Athari za mabadiliko ya tabianchi zimeonekana katika sekta mbalimbali za uzalishaji nchini ikiwemo sekta za Kilimo, Mifugo, Maji, Nishati, Maliasili, Miundombinu na Usafirishaji. Athari hizi ni pamoja na matukio ya ukame; mafuriko; maporomoko ya udongo; ongezeko la joto; kuibuka na mlipuko wa magonjwa ya mazao, mifugo na binadamu; na uwepo wa viumbe vamizi. Jamii maskini hasa za vijijini huathiriwa zaidi na mabadiliko ya tabianchi.

Katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais inaratibu utekelezaji wa Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mifumoikolojia Vijijini.

Mradi huu ni wa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia 2018 hadi 2022 na umefadhiliwa na Mfuko wa Mazingira Duniani (Global Environment Facility – GEF) kwa gharama ya Dola za Marekani 7,571,233 sawa na shilingi 17,413,835,900.

**Lengo la mradi:**
Lengo la Mradi ni kuongeza uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika jamii za vijijini kwa kuimarisha mifumoikolojia na shughuli mbadala za kujiongezea kipato.

**Malengo mahsusi:**

1. Kujenga uwezo wa Wadau kuhusu njia na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia Mifumoikolojia (Ecosystem-based Adaptation).

2. Kuimarisha uwezo wa jamii kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kuimarisha mifumo ikolojia na kupunguza umaskini kupitia: kilimo/ufugaji kinachohimili mabadiliko ya tabianchi (Climate Smart Agriculture); shughuli mbadala za kujiongezea kipato; upatikanaji wa maji; matumizi ya majiko banifu; hifadhi ya misitu na upandaji miti na kuongoa maeneo yaliyoharibika na nyanda za malisho.

3. Kuimarisha upatikanaji wa taarifa na elimu kwa umma kuhusu mbinu bora za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mifumo ikolojia.

**Mradi unatarajiwa kuwafikia takriban**

**1,468,035**

**wanufaika (au kaya 298,631) katika wilaya hizo zenye jamii za wakulima wanaojihusisha kwa kiasi kikubwa na ufugaji.**

# Maeneo Ya Mradi

Mradi unatekelezwa katika mikoa minne Tanzania Bara na mkoa mmoja Tanzania Visiwani. Wilaya hizo na mikoa yake ni wilaya ya Simanjiro mkoa wa Manyara, wilaya ya Kishapu mkoa wa Shinyanga, wilaya ya Mvomero mkoa wa Morogoro, wilaya ya Mpwapwa mkoa wa Dodoma na wilaya ya Kaskazini A mkoa wa Unguja.




© VPO - EBARR Project


**Kaskazini-A, Zanzibar**

**Boti za uvuvi zilizonunuliwa kusaidia uvuvi endelevu kwa jamii huko Kaskazini A, Zanzibar**





**Vikundi vya wanawake kutoka Kijini, Mbuyutende na Jugakuu wakishiriki katika mafunzo ya utengenezaji sabuni**




Josho lililojengwa katika Kijiji cha Ng'hambi wilaya ya Mpwapwa, mkoani Dodoma.

# Mpwapwa, Dodoma



Kisima kirefu kimechimbwa kuhakikisha upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kilimo na mifugo.

# Mvomero, Morogoro




Elimu ya upandaji miti katika shule ya msingi Lubungo wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro.




Ujenzi wa skimu ya umwagiliaji ya Lukenge katika wilaya ya Mvomero, mkoa wa Morogoro.

## Simanjiro, Manyara






Nyumba/banda darasa lililojengwa na vifaranga kutolewa kusaidia ufugaji kuku katika kijiji cha Jitegemee katika wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara




Uoteshaji wa vitalu vya miti katika kijiji cha Orkesmet wilaya ya Simanjiro mkoa wa Manyara

## Kishapu, Shinyanga




Kiwanda kidogo cha kutengeneza bidhaa za ngozi katika kijiji cha Kiloleli wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga




Kwangu Mabambala, mnufaika wa majiko banifu katika wilaya ya Kishapu, mkoa wa Shinyanga.

# Mafanikio ya mradi



© VPO - EBARR Project

# Mafanikio ya mradi

- **76** — Idadi ya watoa maamuzi na wataalam waliopatiwa mafunzo juu ya njia za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mifumo ikolojia (EbA)
- **3** — Mashamba darasa yaliyoanzishwa Kishapu, Mpwapwa, na Mvomero.
- **2** — Majosho yaliyojengwa Simanjiro na Mpwapwa
- **2** — Mabwawa ya maji ya ng’ombe yaliyojengwa Simanjiro na Mpwapwa
- **12** — Visima vilivyochimbwa na kujengwa Mpwapwa, Mvomero, Simanjiro na Kaskazini A.
- **6** — Boti za uvuvi zilizonunuliwa Kaskazini A.
- **2** — Nyumba /mabanda darasa ya kuku yaliyojengwa Simanjiro

# Mafanikio ya Mradi

**2** Viwanda vidogo vya kutengeneza bidhaa za ngozi vilivyojengwa Simanjiro na Kishapu

**850** Vifaranga vya kuku vilivyonunuliwa ili kusaidia vikundi vya ufugaji kuku Simanjiro

**50** Mbuzi mbegu ya Isiolo (Isiolo breed) walionunuliwa Simanjiro

**24** Ng'ombe mbegu ya Borani (Boran breed) walionunuliwa Simanjiro

**400** Mizinga ya nyuki iliyonunuliwa na kusambazwa kwa vikundi vya mradi Kishapu na Simanjiro

**16** Mashimo ya nyuki/nyumba zilizojengwa Kishapu

**650** Urefu wa mita zilizojengwa kutoka mrefeji mkuu wa skimu ya umwagiliaji ya Lukenge Mvomero kuelekea katika mashamba ya jamii (mita 2100 zaidi zinatarajiwa kujengwa)

**78,000** Idadi ya hekta zilizoainishwa kwa ajiili ya mifugo na uhifadhi wa maji kupitia mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji 13 vilivyo ndani ya mradi

**2954** Idadi ya hekta zilizotengwa kwa ajili ya kuhifadhiwa ili kurejesha uoto wa asili kupitia mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji 13 vilivyo ndani ya mradi

**182,416** Idadi ya miti iliyozalishwa katika vitalu katika maeneo yote ya mradi

**1516** Nyumba zilizojengewa majiko banifu

**17** Vijiji vilivyotengenezewa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi

**273** Machapisho ya kukuza uelewa yaliyotayarishwa (ikiwemo vipindi vya radio, vipindi vya runinga, vidokezo katika mitandao ya kijamii, mabango na Mkakati wa Mawasiliano wa Mradi)

**365** Wananchi katika maeneo ya mradi walioshiriki katika mikutano ya kukuza uelewa kuhusu mradi wa EBARR

**2000+** Wananchi wanaojihusisha na vikundi vya uzalishaji mali

**60%**

**Asilimia ya maendeleo ya mradi kwa ujumla 2021 - 2022**



**Kwa mawasiliano:**
**Katibu Mkuu,**
**Ofisi ya Makamu wa Rais,**
**Mji wa Serikali – Mtumba,**
**S.L.P 2502,**
**40406 DODOMA**
**(255) (22) 2163400-19 | (255) (75) 6140140**
**ps@vpo.go.tz**

© VPO - EBARR Project